JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA**

Kumb.Na. **MDC/ADM/10/30/VOL 1/96** 22/07/2024

**YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kwa kuzingatia kibali cha ajira mpya mwaka wa fedha 2023/2024 cha tarehe **25 Juni, 2024** chenye **Kumb Na. FA.9787/288/01/09** kilichotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Maswa anatangaza nafasi za kazi ya **Mtendaji wa Kijiji Daraja la III** na **Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II** kwa Masharti ya kudumu, hivyo watanzania wote wenye sifa hizo mnakaribishwa kutuma maombi ya kujaza nafasi hizo kama ifuatavyo: -

**1.0 MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA III (NAFASI 15)**

**1.1 MAJUKUMU YA KAZI**

i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikari ya Kijiji;
ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamjzi wa Utawala Bora katika Kijiji;
iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji;
iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji;
v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu;
vi. Kuandaa Taarifa ya Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali;
vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo Kitaalam katika Kijiji;
viii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, 163 BR. Uhuru 39382 Maswa, Mkoa wa Simiyu, S.L.P. 170, Maswa
Simu: +255282750271 Nukushi: +255282750376 Barua pepe: ded@maswadc.go.tz Tovuti: www.maswadc.go.tz

ix Mwenyekiti wa Kikao cha Watalaamu waliopo katika Kijiji;

x Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi

xi Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogondogo za Kijiji na;

xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

### 1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu Elimu ya kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu Mafunzo ya Astashahada (Cheti) **NTA Level 5** katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya jamii na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA

Ngazi ya mshahara wa Serikali TGS B.

### 1.2.1 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II (NAFASI 02)

### 1.2.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kuorodhesha barua zinazoingia masjala kwenye rejista.
ii. Kuboresha barua zinazotoka nje ya Halmashauri.
iii. Kusambaza majalada kwa Watendaji (Action Officers)
iv. Kupokea majalada yanayorudi masjala kutoka kwa Watendaji (Action Officers)
v. Kurudisha majalada kwenye kabati la majalada.
vi. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Halmashauri.

### 1.2.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Wahitimu wa kidato cha nne au sita wenye cheti cha **[NTA Level 6]** au Stashahada katika fani ya masjala kutoka vyuo vinavyotambuliwa na na Serikali na wenye ujuzi wa kompyuta.

### 1.2.3 NGAZI YA MSHAHARA

Ngazi ya mshahara wa Serikali **TGS C**

### MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45;
ii. Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuanisha kwenye mfumo wa kuombea ajira aina ya ulemavu walionao.
iii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/ Wakili;

iv. Waombaji ambao tayari ni watumishi wa Umma na wamejipatia sifa zakuingilia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa Waajiri wao na Waajiri wajiridhishe ipasavyo.

v. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika.

vi. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/ Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

vii. Testmonials Provisional Results Statement of Rusults hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.

viii. Waombaji walisoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).

ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

x. Waombaji watakao wasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria.

xi. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **06/08/2024** saa 09:30 Alasiri.

xii. Muhimu: Kumbuka Kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu.Barua zote za maombi ziandikwe kwa;

**Mkurugenzi Mtendaji (W),**

**S.L.P 170,**

**MASWA**

***Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal kupitia anuani ifuatayo: https://portal.ajira.go.tz Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sektretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa "Recruitment Portal'***

**xiii.** Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATASHUGHULIWA.**

Imesainiwa na:-

**Maisha S. Mtipa**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**HALMASHAURI YA WILAYA**
**MASWA**